



# HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE JIMBO LA KISARAWE



## TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA WAPIGA KURA JIMBO LA KISARAWE

Afisa Mwandikishaji Jimbo la Kisarawe anapenda kuwatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa ajili uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2025, litaanza Tarehe **13 Februari 2025** hadi **19 Februari 2025** katika vituo vya uboreshaji vilivyopo kwenye Kata zote katika Jimbo la Kisarawe.

Kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Uboreshaji wa Daftari utahusisha kuandikisha watu wote wenye sifa, Wapiga kura wanaorekebisha au kubadili taarifa, wanaohamisha taarifa, waliopoteza au kadi zao kuharibika na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa.

Mtu atakuwa na sifa za kuandikishwa iwapo;

- (a) *Ni raia wa Tanzania*
- (b) *Ametimiza umri wa miaka kumi na nane na kuendelea;*
- (c) *Aliyehama kutoka eneo moja kwenda eneo jingine*
- (d) *Atatimiza umri wa miaka kumi nane kabla au ifikapo siku ya uchaguzi;*
- (e) *Ni mkaazi wa kawaida katika jimbo au kata ambayo anaomba kuandikishwa;*
- (f) *Ana akili timamu;*
- (g) *Hajatiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au hatumikii kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita;*
- (h) *Hajawekwa kizuizini kwa amri ya Rais; na*
- (i) *Hana uraia wa nchi nyingine tofauti na Tanzania*
- (j) *Wale wote wenye Vitambulisho vilivyotolewa kabla ya Mwaka 2015*

Tujitokeza kushiriki zoezi hili muhimu.

Beatrice R. Dominic  
**AFISA MWANDIKISHAJI**  
**JIMBO LA KISARAWE**



**"KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA"**